Mwanachama wa Hazina SACCOS Ltd ni mtu anayechangia Akiba kila mwezi katika chama hiki. Je, mtu yeyote anaweza kuwa mwanachama wa HAZINA SACCOS LTD?

HAPANA ila ni mtu yeyote ambaye ni mtumishi wa umma Tanzania

## JINSI YA KUJIUNGA NA HAZINA SACCOS LTD

kujaza fomu ya kujiunga inayopatikana ofisi za Hazina SACCOS LTD au kwenye tovuti ya chama

- Kulipa Ada ya kiingilio Tsh 100,000/=
- Kulipa angalau Hisa 25@ 20,000/=
- BIMA YA MKONO WA POLE: Mwanachama mgeni atapaswa kulipa Tsh. 32,400 ikiwa ni gharama za bima mkono wa pole kwa mwaka husika

## HUDUMA ZA KIFEDHA

Mwanachama anaruhusiwa kuweka Akiba (savings) au kulipa deni la Hazina SACCOS Ltd kupitia Benki. Malipo yoyote yanayofanyika kwa mwanachama huwa kwa njia ya Hundi au kwenye akaunti yake

Jina la Akaunti :Hazina Savings and Credit Society Ltd, Akaunti namba: 0150237286200 Benki ya CRDB, Tawi la Holland. 20106600494 Benki ya NMB, Tawi la Bank House.

## UKOMO WA UANACHAMA

Kuhamia Sekta au makampuni binafsi.
Kuacha/kufukuzwa kazi Serikalini /Taasisi.

## KANUNI YA KUTAFUTA RIBA

RIBA =(P (N+1)r)/200

## KIELELEZO

P- MKOPO
N- MUDA WA KUREJESHA MKOPO
R-RATES (0.84% Au 1.5%)

## MAADILI YA HAZINA SACCOS

Uadilifu na Uaminifu
Kutoa Huduma nzuri na zenye ubora kwa wanachama.
Umoja na Ushirikiano.

- Kubuni, kuboresha, kutoa huduma na Bidhaa Bora kwa wanachama.
- Haki na usawa katika kuwahudumia wanachama.
- Kupiga vita rushwa kwa nguvu zote.
- Kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii.
- Kuendesha Saccos kwa misingi ya Uwazi na uwajibikaji.
- Kuheshimu Usawa wa jinsia katika Uongozi wa Saccos.

## WADAU:

| |
|---|
| Wizara mbalimbali Tanzania Bara |
| Halmashauri |
| Mrajis vyama vya ushirika |
| SCCULT (1992) LTD |
| ACCOSCA |
| TCDC,NMB,CRDB,DCB |
| NBC,Tanzania CEO round table |
| FINTECH society of Tanzania |

## KWA MAWASILIANO NA MAELEZO ZAIDI, TAFADHALI WASILIANA NASI KUPITIA ANWANI IFUATAYO:


MWENYEKITI
HAZINA SACCOS LTD, S.L.P 9111, DAR ES SALAAM
TEL: 0222126431, +255 710 933 944 / +255 710 606 605





Hazinasaccos_tz Hazina saccostz Hazinasaccostz info@hazinasaccos.co.tz
info@hazinasaccos.co.tz www.hazinasaccos.co.tz


# HAZINA SACCOS LTD

"Huduma Bora kwa Wakati na Riba Nafuu"



REG: PRI-DAR-DAR-CC-2022-469

## HAZINA SACCOS NI NINI?

Ni Ushirika wa Akiba na Mikopo kwa ajili ya kuinua kustawisha na kuboresha hali za Wanachama wake.

## Historia

Ushirika huu ulianzishwa mwaka 1972 ikiwa na wanachama 100 na kusajiliwa rasmi tarehe 21.03.1973 ikiwa na wanachama 250.

## Dira

Kulinda misingi ya ushirika kwa kutoa huduma bora zinazo kidhi mahitaji na changamoto za wanachama kwa wakati na gharama nafuu

## Dhamira.

kuwa ushirika wa fedha wenye nguvu kwa kukidhi mahitaji ya wanachama kwa huduma na mazao bora

## KWANINI NIJIUNGE HAZINA SACCOS?

HAZINA SACCOS inatoa huduma bora kwa wakati na riba nafuu.

Hazina SACCOS hutoa huduma bora kwa wakati kama.

- Mikopo ya Dharura.
- Mikopo ya waajiriwa wapya
- Mikopo ya kulipia Ada kwa mwanachama, mtoto au tegemezi yeyote anayemuhusu mwanachama.
- Mikopo ya kufanyia Maendeleo ya Biashara au Ujenzi.
- Kukopa kwa ajili ya huduma za misiba kwa wale wanaowahusu wanachama wa hazina Saccos.
- Mikopo ya viwanja.
- Inalipa riba kwenye Akiba za wanachama.
- Inatoa gawio kwa wanachama baada ya kupitishwa na Mkutano Mkuu
- inatoa elimu ya ushirika kwa wanachama wote

## Huduma zitolewazo:

## 1.Utunzaji wa Akiba

Chama hupokea na kutunza Akiba za wanachama kupitia makato kwenye mshahara ,au mwanachama anaweza kulipia bank kiasi chochote Zaidi ya makato anayokatwa katika mshahara wake, aidha chama Kinalipa 1%-5% ya Akiba za mwanachama alizo weka kwa mwaka.

## 2.Utunzaji wa Hisa

Chama hupokea hisa za msingi na hisa za hiari. Mwanachama anaruhusiwa kupunguza au kuhamisha hisa za hiari.

## Hazina Saccos inatoa mikopo ya aina mbalimbali.

- Mkopo wa Dharura.
- Mkopo wa Dharura 2.
- Mkopo wa Ajira Mpya.
- Mkopo wa Tulizamoyo.
- Mkopo wa Elimu.
- Mkopo wa mazishi.
- Mkopo wa sikukuu
- Mkopo wa maendeleo.
- Mkopo wa biashara.
- Mkopo wa ujenzi
- Mkopo wa standing order
- Mkopo wa Fastanatoboa
- Mkopo wa Viwanja.

## Mkopo wa dharura

Kiwango cha juu cha mkopo huu ni Tsh 5,000,000/= na kutoza riba ya 1.5% kwa mwezi. Muda wa juu wa marejesho ni miezi 12, mkopo huu unatolewa ndani ya masaa 24 baada ya kukamilisha taratibu za maombi.

## Mkopo wa dharura 2

Kiwango cha juu cha mkopo huu ni Tsh 10,000,000/= na kutoza riba ya 1.5% kwa mwezi. Muda wa juu wa marejesho ni miezi 24, mkopo huu unatolewa ndani ya siku 7 baada ya kukamilisha taratibu za maombi.

## Mkopo wa Ajira Mpya

Kiwango cha juu cha mkopo huu ni Tsh. 5,000,000/= na kutoza riba ya 1.5% kwa mwezi,muda wa kurejesha ni miezi 18, mkopo huu hutolewa ndani ya masaa 24 baada ya kukamilika kwa maombi ya mkopo

## Mkopo wa Tulizamoyo

Kiwango cha mkopo huu ni kuanziaTsh 300,000/= hadi Tshs 1,000,000/=. Bila Riba
Gharama za kuchakata mkopo ni 5% za kiwango cha mkopo.

## Mkopo wa Elimu

Kiwango cha juu cha mkopo huu ni Tsh 5,000,000 na kutoza riba ya 0.42% Muda wa kurejesha mkopo ni miezi 24. Fomu hupokelewa kuanzia Tarehe 1-20 ya kila mwezi.

## Mkopo wa Mazishi

Kiwango cha juu cha mkopo huu ni Tsh. 3,000,000 na kutoza riba ya 0.42%% muda wa kurejesha ni miezi 24, mkopo huu hutolewa pale mwanachama anapokua amefiwa na mtu yoyote

## Mkopo wa Sikukuu

Kiwango cha juu cha mkopo huu ni 500,000/= na kutoza riba ya 0.84%. Muda wa juu wa kureje-sha mkopo huu ni miezi 6 Hutolewa kwa sikukuu za krismasi, Pasaka na Idd El-fitri.

## Mkopo wa Maendeleo

Kiwango cha juu cha mkopo huu ni mara tatu (3) ya Akiba hadi shilingi milioni mia moja na kutoza riba ya 0.84%. Muda wa kurejesha ni miezi 12 - 60 Hutolewa mwishoni mwa mwezi na fomu hupokelewa kuanzia tarehe 1-20 ya kila mwezi.

## Mkopo wa Biashara

Kiwango cha juu ni mara tatu (3) ya Akiba hadi shilingi milioni mia moja na kutoza riba ya 0.84% .kwa mwezi Muda wa marejesho ni miezi 12-60. Fomu huanza kupokelewa kuanzia tarehe 1-20 ya kila mwezi.

## Mkopo wa Ujenzi

Kiwango cha juu ni mara 3 ya akiba hadi shilingi milioni mia moja na riba ya 0.84% Muda wa marejesho ni miezi 12-60 fomu hupokelewa kuanzia tarehe 1-20 ya kila mwezi.

## Mkopo wa utaratibu wa Bank (Standing Order)

Kiwango cha juu ni Tsh 50,000,000.00 na kutoza riba ya 1.5% muda wa kurejesha ni miezi 48 fomu hupokelewa kuanzia tarehe 1-20 ya kila mwezi.

## Mkopo wa Fastanatoboa

Kiwango cha juu ni Tsh 5,000,000/= na kutoza riba ya 1.40% kwa mwezi muda wa marejesho ni miezi 5 na hutolewa ndani ya masaa 12 baada ya kukamilika kwa taratibu za maombi.

## Mkopo wa Viwanja

Hutegemea na taratibu zitakazowekwa na chama kwa wakati huo.